# Tunakuletea Habari kuhusu AZERBAIJAN

**Musa MARJANLI,**
**Mhariri mkuu**

Wasomaji wapendwa, tuna furaha kukutana nanyi kwa mara ya kwanza na tunatumai tutaendelea kukutana zaidi kwa manufaa ya pande zote. Jarida la IRS limechapishwa katika lugha 20 kufikia sasa, na toleo la Kiswahili limezinduliwa. Hili ni tukio muhimu, kwa sababu kufikia sasa jarida letu lilikuwa likichapishwa tu nchini Ethiopia, kwa lugha ya Kiamhara, barani Afrika. Jarida la IRS ni chapisho la kimataifa lenye makao yake nchini Azerbaijan, nchi inayopatikana katika eneo la Caucasus kwenye makutano ya bara Ulaya na bara Asia, na husambaza habari muhimu kuhusu historia, utamaduni, na maisha ya kisasa ya watu wa Azerbaijani. Nchi yetu ilipata upya uhuru wake mwaka wa 1991 baada ya kuvunjika kwa Muungano wa Kisovieti, na tangu wakati huo tumestahimili changamoto nyingi, zikiwemo kunyakuliwa kwa muda mrefu kwa sehemu ya eneo letu na nchi jirani ya Armenia. Kufikia sasa, changamoto hizi na nyingine nyingi zimepita na Azerbaijan imepiga hatua kubwa za kimaendeleo. Azerbaijan pia ni msambazaji mkuu wa mafuta na gesi katika masoko ya kimataifa na ina jukumu muhimu la kuhakikisha usalama wa kawi barani Ulaya. Ikiwa na idadi kubwa ya Waislamu, Azerbaijan pia ilikuwa moja ya nchi za kwanza kukubali dini za Wakristo na Wayahudi. Wawakilishi wa makabila na dini mbalimbali wameishi humu nchini kwa amani na ujirani mwema kwa miaka mingi. Katika miaka ya hivi karibuni, Azerbaijan imekuwa ikizingatia sana kukuza mahusiano na nchi za Afrika. Makala yaliyoandikwa na Balozi wa nchi yetu nchini Kenya, Sultan Hajiyev, yanahusiana na mada hii. Unaweza pia kusoma kuhusu ukarabati na kujengwa upya kwa maeneno yaliyokua yamenyakuliwa.

Katika toleo hili la kwanza, tumeamua kulenga usanifu majengo na maendeleo ya miji, tukizingatia kuwa nyanja hii imepewa kipaumbele nchini Kenya. Tunawaleteeni wasomaji wetu habari kuhusu maendeleo ya miji na majengo muhimu zaidi ya kiusanifu ya Baku, mji mkuu wa Azerbaijan: Icherisheher, ngome ya enzi za kati na kiini cha kihistoria cha mji mkuu, na Kituo cha Heydar Aliyev, mjengo wa usanifu wa kisasa wa aina yake ambao si tu muhimu kitaifa lakini pia kimataifa. Ninatumai utagundua jambo jipya katika toleo hili na matoleo ya baadaye ya jarida letu, na ninakuhimiza uendelee kutufuatilia.